Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili - 00005809 Toleo 18: Juni, 2015

Huduma bora za afya kwa watanzania wote

Muuguzi katika moja ya zahanati wilayani Mpwapwa akionesha baadhi ya dawa.

Utangulizi

Toleo hili la 18 linaelezea kwa ufupi baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Sikika katika robo ya pili ya mwaka 2015.

Katika kipindi hiki, tulifanya uchambuzi wa bajeti na kugundua kuwa kiasi cha bajeti ya nchi kilichotengwa kwa ajili ya dawa muhimu na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kwa mwaka 2015/16, imeshuka kwa asilimia 48 kutoka bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15.

Shirika pia lilishirikiana na wadau wengine kutoa tuzo za umahiri katika uandishi wa habari nchini kwa mwaka 2014 (EJAT), ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa waandishi wa habari katika kukuza utamaduni wa uwazi, uwajibikaji na utawala bora, hususan kwenye sekta ya afya.

Baada ya zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (SAM) 2013, tulishuhudia uboreshwaji wa huduma za afya wilayani Kibaha, mkoani Pwani. Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya wilayani humo viliongeza makusanyo ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kutoka Tsh 18,934,000/- kwa mwaka 2013 na hadi kufikia Tsh 55,440,000/- kwa mwaka 2015.

Pia, kituo cha afya Mlandizi, kilichopo wilayani humo kilianza kushughulikia mifumo ya kutolea malalamiko tofauti na awali ambapo kituo hicho kilikabiliwa na changamoto ya kupata maoni kutoka kwa wagonjwa.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kazi za Sikika, tafadhali peruzi tovuti yetu; *www.sikika.or.tz*, twitter - *@sikika1*, facebook - *Sikika Tanzania* na blogspot - *www.sikika-tz.blogspot.com.* Kwa maoni tafadhali wasiliana nasi kupitia *info@sikika.or.tz* au sms *0688-493-882*.

NDANI

Bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba kiini macho! 2
SAM yachangia makusanyo CHF Kibaha 3
Mlandizi yaboresha mifumo ya utoaji malalamiko 3
Sikika yashiriki Tuzo za EJAT 4

Bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba kiini macho!

Na Alice Monyo

Baadhi ya wagonjwa wakichukua Dawa katika Kituo cha Afya, Mlandizi.

BAJETI ya nchi iliyotengwa kwa ajili ya dawa muhimu na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kwa mwaka 2015/16, imeshuka kwa asilimia 48 kutoka bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 yaani kutoka Tsh 70.5 billioni mpaka Tsh. 39 billioni.

Uchambuzi wa bajeti katika kipindi cha miaka miwili iliyopita 2013/14 na 2014/15 unaonesha kwamba mahitaji halisi ya dawa muhimu na vifaa tiba yalikuwa ni shilingi bilioni 549 na shilingi bilioni 577, wakati bajeti iliyotengwa ni shilingi bilioni 64 (2013/14) na shilingi bilioni 70.5 (2014/15).

Kushuka huko kwa bajeti kunamaanisha kwamba kila mtanzania amepangiwa wastani wa shilingi 1,000/- kwa mwaka, kwa ajili ya dawa muhimu na vifaa tiba. Kwa mujibu wa sensa ya taifa, Tanzania ina watu takribani milioni 47. Kwa bajeti ndogo kama hii, tutapunguza vipi tatizo sugu la upungufu na ukosefu wa dawa muhimu na vifaa tiba nchini?

Moja ya sababu za msingi ya upungufu na ukosekanaji wa dawa nchini ni ufinyu wa bajeti inayotengwa mwaka hadi mwaka. Upungufu na hata ukosefu wa dawa muhimu na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma umekuwa ukijitokeza mara kwa mara hapa nchini. Hali hii inachangia kuzorota kwa huduma za afya ambapo waathirika wakuu ni wananchi wa hali ya chini.

Zaidi, tathmini ya upatikanaji na utayari wa huduma uliofanywa na Taasisi ya Utafiti ya Ifakara, inaonesha kuwa, upatikanaji wa dawa muhimu nchini kwa mwaka 2012 ulikuwa asilimia 41 tu (MOHSW, 2013). Hii ina maana kuwa, karibu asilimia 60 ya dawa muhimu hazikuwepo katika vituo vya kutolea huduma za afya katika kipindi hicho.Tukumbuke kuwa mwaka 2012 bajeti ya dawa na vifaa tiba ilikuwa zaidi ya billion 100, je upatikanaji wa dawa nchini utakuwaje mwaka huu ambao bajeti ni pungufu ya nusu ya bajeti ya mwaka 2012?

Pia ni vema kujiuliza, bajeti hii inawezaje kufikia lengo la mkakati mpya wa serikali wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)? Lengo la BRN ni kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba unafikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2016. Je, bajeti hii imezingatia mambo muhimu kama ongezeko la watu, ongezeko la vituo vipya vya kutolea huduma, magonjwa na hata mahitaji halisi ya dawa?

Aidha, moja ya mikakati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuziba pengo linalotokana na bajeti hiyo ndogo ni kutumia mapato yatokanayo na uchangiaji huduma za afya pamoja na vyanzo vingine vya halmashauri ili kununua dawa muhimu na vifaa tiba. Hata hivyo, kutumia fedha za uchangiaji ili kuziba pengo lililopo kwa mwaka 2015/16 itakuwa ni vigumu kutokana na ukubwa wa mahitaji ukilinganisha na mapato ya uchangiaji.

Kwa mfano, ni asilimia 20 tu ya watanzania wote wanachangia huduma za afya kupitia bima za afya hivyo asilimia 20 ya watanzania hawawezi kukusanya fedha za kutoshelezea mahitaji ya dawa muhimu na vifaa tiba ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 577. Pamoja na hayo, bado kuna mapungufu katika miongozo ya matumizi ya fedha za uchangiaji. Hivyo, itakuwa vigumu kwa sasa kutegemea vyanzo hivyo kama mkombozi wa kutatua changamoto za upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba nchini.

Fedha hizo za uchangiaji zinaweza kuwa ni moja ya mikakati ya muda mrefu ya kutatua tatizo la uhaba wa dawa muhimu na vifaa tiba lakini sio mkakati wa dharura kama ilivyo sasa. Hivyo, serikali inapaswa kuboresha mifumo ya uchangiaji kabla ya kuanza utekelezaji wake.

Tunashauri serikali kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya dawa muhimu na vifaa tiba zinatolewa zote na kwa wakati kwenda Bohari Kuu ya Dawa ili kuondoa upungufu wa dawa muhimu na vifaa tiba nchini. Vilevile, serikali ione ni namna gani itaweza kuziba pengo la upungufu wa bajeti kwa mwakahuu wa fedha 2015/16.

SAM yachangia makusanyo CHF Kibaha

Na Beatrice Mkani, Kibaha

WILAYA ya Kibaha imepiga hatua katika makusanyo ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kutoka Tsh 18,934,000/- kwa mwaka 2013 na hadi kufikia Tsh. 55,440,000/- kwa mwaka 2015.

Hiyo imechangia mkoa wa Pwani kuongoza na pia kushika nafasi ya nne kitaifa baada ya kuvuka malengo ya taifa ya makusanyo na matumizi ya fedha za mfuko huo kuanzia mwaka 2013. Hadi kufikia 2015, wilaya hiyo iliweza kukusanya 59% ya jumla ya kaya zote wilayani humo ukilinganisha na malengo ya serikali ambayo ni 30% kwa jumla ya kaya zote kwa kila wilaya.

Mfuko huo kwa kiasi kikubwa umechangia uwepo na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya Afya na zahanati wilayani humo. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo kutoka Halmashauri unaonesha kuwa 67% inatumika kununua dawa, 15% kwa ajili ya vifaa tiba na zilizobaki ni kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya na kulipa posho za wajumbe wa kamati za afya.

Hali hii imeiwezesha Kibaha kukabiliana na upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba ambao umekuwa ukisababishwa na bajeti ndogo kutoka Serikali kuu, ucheleweshwaji na uhaba wa dawa kutoka Bohari kuu ya Dawa ya Taifa (MSD).

Sikika inaamini kwamba kuboreshwa kwa uendeshaji wa mfuko huo wa afya wilayani humo, kumechangiwa na utekelezaji wa zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (SAM) lililofanyika mwaka 2013. Zoezi hilo liliwawezesha wananchi na wadau wa afya kubaini mapungufu katika uendeshaji wa mfuko huo na kuishauri vyema Halmashauri hiyo jinsi ya kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili.

Mapungufu hayo yalikuwa ni pamoja na kutokuwa na akaunti za vituo vya afya kwa ajili ya utunzaji wa fedha hizo, mlolongo mkubwa wa kuidhinisha matumizi ya mfuko huo ambao ulisababisha kutokuwepo kwa dawa vituoni na kuwakatisha tamaa wananchi kujiunga na kuchangia.

Sikika inawapongeza wananchi na pia uongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Kibaha kwa hatua hiyo na kushauri wilaya zingine kuiga mfano huo ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, hususan kwa upande wa upatikanaji wa dawa nchini.

Mlandizi yaboresha mifumo ya utoaji malalamiko

Na Jackson Sikahanga, Mlandizi

Matatizo ya mifumo ya kutolea na kushughulikia malalamiko ya watumia huduma wanapokwenda kupatiwa matibabu katika kituo cha afya Mlandizi, wilayani Kibaha, mkoa wa Pwani yamepatiwa ufumbuzi.

Uongozi wa kituo cha afya Mlandizi umeboresha mfumo wa kushughulikia malalamiko kwa kuunda kamati huru kwa ajili ya kukusanya, kufuatilia na kushughulikia malalamiko na maoni yanayotolewa na wananchi ili kuboresha huduma za afya. “Kamati hii inaundwa na wajumbe wanne (4) ikijumuisha wauguzi wawili, mjumbe kutoka kwenye jamii na mwingine kutoka TALGWU (Tanzania Local Government Workers Union).”

Mganga mfawidhi wa kituo hicho Bw. Adronicus Aloyce Rwelamila alifafanua kwa kusema “kamati hiyo hukutana mara moja kila mwezi kwa lengo la kufungua masanduku ya maoni, kujadili na kisha kutoa mapendekezo kwa uongozi wa kituo kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki juu ya malalamiko yaliyowasilishwa na wananchi.”

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mlandizi Dkt. Adronicus Aloyce Rwelamila akieleza baadhi ya mafanikio katika kituo hicho yaliyotokana na timu ya SAM - Kibaha.

“Karibu kila jengo zikiwemo ofisi za utawala, zimewekewa masanduku ambayo hutumiwa na wananchi kutoa maoni yao juu ya huduma zinazotolewa kituoni hapa…kwa ujumla tuna masanduku kumi”. Aliongeza Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho cha afya.

Aidha ufanisi wa mifumo hiyo hupimwa kwa kuangalia ni kwa kiwango gani wananchi wanawasilisha malalamiko yao na jinsi yanavyopatiwa ufumbuzi ili kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya. Kwa kawaida, wananchi watashawishika kutoa maoni / malalamiko yao pindi wanapoona yanafanyiwa kazi kwa wakati na matokeo yake yanaonekana machoni pa watumia huduma. Hii huongeza uaminifu kwa watumia huduma juu ya mifumo iliyopo na huongeza uwazi na uwajibikaji kwa watoa huduma.

"Kwa mfano, zamani kadi za CHF tulikuwa tunachukulia kwenye jengo la CTC, tuliwasilisha malalamiko yetu kupitia masanduku ya maoni kama unavyoyaona kwenye hizo kuta, baada ya kuona ni usumbufu huduma upate sehemu nyingine - kadi ukachukue sehemu nyingine. Lakini tunaushukuru utawala wameshughulikia na sasa hatuchukulii kule CTC tena" aliongeza mmoja wa wagonjwa.

Tunaupongeza uongozi wa Halmashauri ya Kibaha kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo. Tunashauri vituo vingine vya kutolea huduma za afya wilayani humo pia viboreshe mifumo ya utoaji malalamiko na namna ya kuyashughulikia.

Sikika yashiriki Tuzo za EJAT

Na Thomas Ludovick

Mkurungenzi wa Sikika Bw. Irenei Kiria akimkabidhi tuzo Tuma Dandi kutoka Mlimani Radio baada ya kuibuka mshindi kwenye Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za EJAT 2014, katika kuripoti habari za afya kwa upande wa radio.

Mwanzoni mwa robo hii ya pili, Sikika ilishirikiana na wadau wengine kutoa tuzo za umahiri katika uandishi wa habari nchini kwa mwaka 2014 (EJAT), ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa waandishi wa habari katika kukuza utamaduni wa uwazi, uwajibikaji na utawala bora hususan katika sekta ya afya.

Kipengele cha habari za afya ni miongoni mwa tuzo 21 zilizoshindanishwa katika tukio hilo lililofanyika Aprili 24, mwaka huu, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Makamu wa Rais, Dk Mohammed Gharib Bilal. Sikika ilitoa tuzo ya mwandishi bora wa habari za afya kwa upande wa radio iliyotwaliwa na Bw. Tuma Dandi kutoka Mlimani Radio.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika Bw. Irenei Kiria alitumia fursa hiyo kumuomba Rais Jakaya Kikwete kutosaini miswada miwili ya Takwimu na ule wa Mitandao mpaka hapo baadhi ya vipengele vinavyozuia wananchi kupata haki ya habari vitakapofanyiwa marekebisho.

"Tunamuomba Rais kutosaini miswada hii miwili ambayo ni muhimu kwa wananchi mpaka hapo wadau watakaposhirikishwa kikamilifu katika kuboresha miswada hiyo," alisema Bw. Kiria.

Naye, Makamu wa Rais, Dk. Mohamed Gharib Bilal, akizumgumzia miswada ya vyombo vya habari alisema nia ya serikali ni njema na imelenga kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na haki ya wananchi kupata habari na taarifa mbalimbali kama msingi wa kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa serikali. "Sheria zitakazosimamia upatikanaji wa haki hizo ni nzuri, hivyo wadau wa habari washiriki kikamilifu kutoa mapendekezo ili kuboresha miswada hiyo," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mukajanga (MCT), alisema ni mwaka wa sita mfululizo kwa Baraza la Habari na washirika wake kutoa tuzo kwa wanahabari. Kwa Sikika huu ni mwaka wa tatu mfululizo kushirikiana na wadau wa habari nchini kuandaa tuzo hizo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688493882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Faksi: 026 23 21316